# Learning by Ear 2009 – "Against the Current" Urban Exodus

## Episode 01: "Without a job, the city is hell"

**Author: Alfred Dogbé**
**Editor: Yann Durand**
**Translator: Anne Thomas**

Wahusika :

Onyesho la 1 :

- **BEN** (MHANDISI WA KILIMO, MWANAMUMEE, UMRI WA MIAKA 29 )
- **KABO** (MKULIMA, MJOMBAKE BEN, MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 57)

Onyesho la 2 :

- **BAKI** (MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YA ZEINA NA BEN, MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 26)
- **ZEINA** (MWANAUCHUMI, RAFIKI YA BAKI NA BEN, MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 24)

Onyesho la 3 :

- **BAKI** (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 26)
- **ZEINA** (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 24)

- **BEN** (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 29)
- 

## Intro:

Karibu kwenye mfululizo mpya wa vipindi vya Learning by Ear kuhusu uhamiaji mijini, uitwao “Kukabiliana na wimbi la mabadiliko”.

Tutafuatiliza masaibu ya Ben na marafiki zake Baki na Zeina. Vijana hao watatu walio na shahada za chuo kikuu wameamua kurudi vijijini kuanzisha chama cha ushirika cha kilimo walipokosa kufanikiwa kujiendeleza mjini.

Ben ana umri wa miaka 29. Ni mhandisi wa kilimo. Ameacha kazi ya utumishi wa umma kwa kuwa hakuweza kuutumia ujuzi wake ipasavyo kuwahudumia wakulima na wanakijiji.

Zeina ana umri wa miaka 24 na ni mwanauchumi. Tangu alipohitimu, amekuwa na matumaini ya kupata ajira ya kudumu na kuishi na kuanzisha familia pamoja na mchumba wake, Baki.

Baki, naye amekata tamaa ya kupata kazi ya kudumu nchini mwake. Ameamua kwenda Marekani atakakotumia uzoefu alioupata kwa kuwa mwanaelimujamii anayeshughulikia mashirika.

Kwenye tukio hili la kwanza utafahamu jinsi vijana hawa, wasio na ajira, wanavyojaribu kulifumbua suala hili moja: Je, vipi tunaweza kujikwamua kutokana na hali hii?

**MUSIC**

**Scene 1: In town. At Ben's home.**

**BEN, KABO**

1. **ATMO : MUSIC PLAYS ON RADIO**

2. **SFX : LEAFING THROUGH A NEWSPAPER**

3. **SFX : KNOCKING AT THE DOOR, ONCE, TWICE AND THEN PERSISTENTLY**

4. **KABO (SHOUTING):** Ben! Ben, Kwani husikii…? Ben!

5. **SFX : RADIO IS TURNED OFF**

6. **SFX : A KEY TURNS IN THE LOCK**

7. **SFX : THE DOOR OPENS**

8. **BEN** Mjomba Kabo! … Hujambo? Nilikuwa nikisikiliza redio. Sijasikia uliponiita. Kwani unarudi kijijini hivi leo?

**9.** **KABO** Naam.

**10.** **BEN** Basi nitakusindikiza hadi kituoni.

**11.** **KABO** Safari bado.

**12.** **BEN** Ungetaka nikuletee chochote kutoka mjini?

**13.** **KABO** Nimekuja kuzungumza nawe.

**14.** **BEN** Karibu ndani, tafadhali!

**15.** **KABO** La! Sikawii. (HE SIGHS). Wajua niliwasili hapa siku tatu zilizopita. Sijakuona hata mara moja ukienda kazini. Nafahamu kwamba umeacha kazi.

**16.** **BEN** Ndiyo, hilo ni kweli. Mjomba, mimi ni mhandisi wa kilimo. Nimesoma kwa kiasi cha miaka 8. Wameniweka kwenye ofisi ambayo haina lolote la kufanya. Wakuu wetu wanatuambia tusiingie kazini pamoja kwani kuna viti viwili, ingawa sisi tuko watano.

**17.** **KABO** Ulifurushwa au uliacha kazi mwenyewe kupenda?

**18.** **BEN** Niliacha kazi mwenyewe kupenda.

**19.** **KABO** Wajua ni watu wangapi wanaotafuta ajira hivi tuongeapo? Zaidi ya nusu ya watu wa kizazi chako watatimia umri wa miaka 40 bila kuajiriwa. Na wewe…

**20. BEN** Nikisalia hapo nitasahau mambo yote niliyojifunza. Ningependa kutumia ujuzi na elimu yangu, kuwasaidia wakulima. Nikibakia hapo sitamfaidi mtu yeyote.

**21. KABO** Na je, utawafaidi watu kwa kushinda umejilaza kitandani mchana kutwa?

**22. BEN** Akh!

**23. KABO** Nisikize kwa makini! Wewe ndiye mtu wa kwanza aliyesoma miongoni mwa jamaa zetu. Mtu wa kwanza kupata cheti cha shule ya msingi kisha cheti cha shule ya upili halafu vyeti vinginevyo uvijuavyo wewe... Tunajivunia kuwa nawe. Ulipokuwa ukija nyumbani na vyeti hivyo, sisi, wajomba zako, shangazi zako, tulikuwa na matumaini kwamba tungeondokana na dhiki na umasikini. Na sasa kubwa unalolifanya ni kujilaza kitandani?

**24. BEN** Mjomba, ninasema …

**25. KABO** Nisikize kwa makini! Hakuna mtu kwenye familia yetu anayekutaka umfanyie kazi. Miaka yote hiyo ulipokuwa shuleni, baba yako alikuhangaikia sana. Hivi sasa amestaafu. Huoni kwamba inambidi apumzike? Unadhani hana haki ya kufurahia hatima ya jasho lake pale anapokuona ukifanya

kazi?

**26. BEN** Nina…

**27. KABO** Usinikate kauli! Mimi na baba yako hatukusoma. Hatukujua ulichokuwa ukikisoma. Lakini wewe ndiye unayetegemewa na familia nzima. Hilo usilisahau hata kidogo! Wewe si mtoto. Lau ingekuwa zamani, ungekuwa shambani ukifanya kazi kuwakimu jamaa zako. Hayo ndiyo niliyotaka kukwambia. Nitarudi zangu kijijini leo usiku. Ningependa kusikia kwamba umeanza kufanya kazi. Fanya vyovyote utakavyo lakini fanya kazi! Zingatia heshima yako.

**28. SFX: ANGRY STEPS WALKING AWAY GRADUALLY**

**29. BEN** Mjomba Kabo! … Mjomba Kabo! (sighs)

**30. SFX: THE DOOR SHUTS. A KEY TURNS IN THE LOCK**

**31. SFX: LOUD AND HEAVY STEPS**

**------- Music -------**

## Scene 2: In town on the street

**BAKI, ZEINA**

**32. ATMO: SOUNDS OF THE STREET: CAR HORNS AND BRAKES ETC…**

**33. BAKI** Zeina mambo!

**34. SFX : TWO HANDS CLAPPING ENTHUSIASTICALLY**

**35. ZEINA** Poa, Baki! Nilikuwa nikija kwako. Hatuonani siku hizi. Kwani umepata kazi?

**36. BAKI** Ndiyo, lakini si kwa muda mrefu. Ilikuwa shughuli ya uchunguzi wa kijamii. Nilikuwa nikimshikilia mtu fulani kazi ya usimamizi.

**37. ZEINA** Na hukupata muda wa kunijulisha kuhusu hilo… Natumai walikupa malipo mazuri.

**38. BAKI** Naam, malipo yalikuwa mazuri.

**39. ZEINA** Basi mbona unalalamika? Sasa unaweza kutulia.

**40. BAKI** Ebu twende Hope Café, nikakununulie kinywaji.

**41. ZEINA** (Teasing) Sidhani kama hilo linatosha kwangu mimi kukusamehe!

**42. BAKI** Usiponisamehe wewe, nani mwengine atanisamehe?

**43. ZEINA** Mimi! (Laughter) Twende zetu!

**44. SFX : STREET SOUNDS FADE OUT-CAFÉ AMBIENCE FADE IN**

**45. SFX : SOUNDS OF STEPS**

**46. ZEINA** Wiki mbili! Nimekuwa nikitamani sana kukuona!

**47. BAKI** Mimi pia!

**48. ZEINA** Nahisi kana kwamba sasa siwezi kuishi bila kuwa na nawe na unataka kwenda…

**49. BAKI** Haya si maisha! Mambo hayafanyiki hivi. Nitasubiri kwa muda gani hata nipate kazi ya kufanya?

**50. ZEINA** Mimi sijafanya kazi kwa muda wa miezi sita. Nimekuwa nikipeleka barua za maombi. Kila mara huitwa kwa mahojiano ya kazi. Wala sijapata kitu. Wiki iliyopita, nilikwenda kwenye kituo cha mafuta ya petroli alikuwa anatakiwa msimamizi. Alinisikiliza, akatizama barua yangu ya maombi ya kazi kisha…..

**51. BAKI** Kisha akakushukuru!

**52. ZEINA** Kunishukuru afadhali! Alitwaa vyeti vyangu vyote akanirejeshea:

**(Imitating the man's voice):**

"Hivi ni vingi sana! Sihitaji vyeti vyote hivi. Hata hivyo msichana kama wewe anaweza kuwavutia wateja. Rudi kesho tutatazama mambo yako." Niliporudi alikuwa ameshamwajiri msichana mwengine ambaye hana ujuzi wowote.

**53. BAKI** Bila shaka! Huyo msichana ni nafuu kwake! Hawezi kudai mambo mengi ilhali wewe unaweza kudai mambo mengine kwa shahada yako hiyo ya uchumi.

**54. ZEINA** Watu hawataki kuutumia ujuzi wa watu wengine kisha hubaki wakilalamika kwamba mashirika yao hayaendeshwi vyema.

**55. BAKI** Huwezi kurekebisha hali hiyo!

**56. ZEINA** Kuna wakati niliongoza kwenye mtihani fulani. Ulikuwa mtihani wa mahojiano ya cheo cha usimamizi wa mradi fulani. Bwana mwenyewe alitaka kunipa kazi…

**57. BAKI** Lakini?...

**58. ZEINA** Kitandani mwake!

**59. BAKI** Mpumbavu huyo! Nimechoka na hali ya mambo nchini mwetu! Nitajitahidi niwezavyo kupata

kandarasi mbili tatu nzuri nipate fedha za nauli ya ndege pamoja na viza.

**60. ZEINA** Huwezi kufanya hivyo!

**61. BAKI** Zeina! Tumeshalizungumzia jambo hili. Hatuwezi kuishi hivi, kukaa kiholela tu hadi kifo chetu kitakapotufika. Inatubidi kujaribu bahati zetu kwengineko. Kazi mbili tatu hivi kisha niondoke.

**62. ZEINA** (sighing) Kwa hisani yako!

**63. BAKI** Nitakapotulizana, nawe unaweza kunifuata. Utaona!

**64. ZEINA** Nini?

**65. BAKI** Hali ya huko itakuwa nzuri kuliko hapa.

Ninakuhakikishia hilo!

**66. ZEINA** Si wazo zuri hilo. Hatma ya maisha yetu ni hapa!

**67. BAKI** Hatma ya maisha yangu ni Marekani.

**68. ZEINA** Unadhani utatosheka kuishi huko?

**69. BAKI** Huko nitapata fursa ya kujitosheleza na kujisimamia mimi binafsi bila kumtegemea mtu.

**70. ZEINA** Hilo si kweli!

**71. BAKI** Sitaki kwendelea kuteseka bure bilashi. Sikubahatika kuajiriwa kwenye sekta ya utumishi wa

umma. Kwa hivyo nitakwenda zangu na kujaribu bahati yangu kwengineko, hilo tu!

**72. ZEINA** Sekta ya utumishi wa umma si kwamba nayo ni nzuri. Ben ameshaacha kazi!

**73. BAKI** Ati nini? Ana akili timamu?

**74. ZEINA** Muulize hayo wewe mwenyewe!

**75. BAKI** Sijamuona kwa muda mrefu. Waonaje tukimtembelea?

**76. ZEINA** Twende!

**77. SFX: STEPS GOING AWAY FAST**

**------ MUSIC ------**

**Scene 3: In town at Ben's house.**

**BEN, BAKI, ZEINA**

**78. ATMO: MUSIC PLAYING ON THE RADIO**

**79. SFX: SOMEONE KNOCKING AT THE DOOR**

80. **BEN** Karibu! Mlango u wazi!

81. **BAKI** Ben, hujambo!

82. **BEN** Baki! Zeina! Habari zenu?

83. **SFX: HANDS CLAPPING WARMLY**

84. **ZEINA** Nzuri!

85. **BAKI** Mbaya!

86. **ZEINA** Na wewe pia? Usiseme hayo. Usijiaibishe!

87. **ZEINA, BAKI, BEN LAUGHTER**

88. **BAKI** Zeina ameniambia kwamba u ...

89. **BEN** Nimeacha kazi. Ni kweli.

90. **BAKI** Kwa nini?

91. **BEN** Nimechoka kupoteza muda wangu. Kaeni!

92. **ZEINA** Asante!

93. **BAKI** Umepanga kufanya nini?

94. **BEN** Ninataka kuanzisha shirika langu mwenyewe.

95. **ZEINA** Fikra nzuri hiyo!

96. **BEN** Nipanga kuanzisha chama cha ushirika cha kilimo.

Nimekuwa kwa muda wa wiki moja nikitayarisha mkakati wa shughuli za chama lakini imekuwa vigumu kuukamilisha.

**97. ZEINA** Baki anaweza kukusaidia. Hayo anayajua sana!

**98. BAKI** Asilimia 95 ya mashirika madogo na yale ya wastani yanayoanzishwa humu nchini husambaratika kabla hayajatimia mwaka wa tatu tangu yalipoanzishwa. Kiwango hicho ni kikubwa hata kuliko kiwango cha vifo vinavyotokea.

**99. BEN** Baki, badala ya kupoteza muda tukisubiri kupewa kazi nzuri zenye mishahara minono kwanini tusianzishe mradi tunaoupenda ambao utawafaa watu wetu?

**100. BAKI** Achana na hilo jambo! Watu wengi wamejaribu. Wote hakuna aliyefaulu!

**101. ZEINA** Sawa, lakini sisi hatujajaribu.

**102. BEN** Sikiliza Baki. Wewe ni mwanaelimu-jamii. Zeina ni mwanauchumi na mimi ni mtaalamu wa kilimo. Tuna ujuzi unaohitajika. Tunaweza kufanikiwa

**103. ZEINA** Ni jambo zuri kulitekeleza. Njia mwafaka ya kujiandalia hatma ya maisha yetu ya siku za usoni.

**104. BAKI** Nimekwambia maisha yangu ni Marekani.

**105. ZEINA** Baki! Tunakuhitaji ubaki hapa.

**106. BEN** Utasoma taarifa ya mkakati ambayo nimejaribu kutayarisha au la?

**107. ZEINA** Tupe uzoefu wako…Tafadhali…

**108. BAKI** Mbona unanitazama hivyo, Ben? Unajua vyema kwamba sitasema ndiyo ili nikuridhishe ,Marafiki hatupaswi kudanganyana, au siyo?... Taarifa yenyewe i wapi?

**109. BEN** Hii hapa! Lakini si safi...!

**110. SFX: PAPER NOISE**

**111. ZEINA** Taratibu nawe, utairarua!

**112. BEN** Sikizeni, Ninakwenda kuitoa nakala mara moja. Kisha nyinyi mtaisoma muwapo na nafasi halafu tutakutana tuijadili

**113. ZEINA** Nadhani kesho ni sawa!

**114. BEN** Naam, kesho. Tukutane Hope Café. Nitagharamia kila kitu!

**115. BAKI** Sawa.

**116. BEN** Ninakwenda kutoa nakala. Msiondoke. Nitarudi hivi

punde!

**117. SFX: STEPS MOVING AWAY FAST**

**118. BAKI** (Sighing) Ninajihisi kama niliyefanya kosa.

**119. ZEINA** Kwa nini?

**120. BAKI** Nimekubali aliloniomba ili kumfurahisha!

**121. ZEINA** Iwapo mradi utakuwa mzuri kama ninavyotaraji, utauridhia uamuzi wako huu.

**122. BAKI** Na ukiwa mbaya?

**123. ZEINA** Tutashirikiana kuuimarisha.

**124. BAKI** Na tusipofanikiwa?

**125. ZEINA** Kwa hali yoyote ile, sitakwenda Marekani.

**126. BEN** Hivyo basi, nitakwangamiza wewe halafu nami nijitie kitanzi!

**127. BEN, ZEINA (BURST INTO LAUGHTER)**

**<u>Outro:</u>**

Na huo ndio mwisho wa kipindi chetu cha Learning by Ear leo hii. Usikose kipindi kijacho ili ujue iwapo Baki na Zeina wanavutiwa na mradi wa Ben, na iwapo Zeina atafaulu kumshawishi Baki asiondoke.

Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutupa maoni yako, fungua ukurasa wetu wa tovuti www.dw-world.de/lbe au utuandikie barua-pepe kupitia anwani lbe@dw-world.de. Kumbuka kusikiliza kipindi kitakachofuata!

**END OF EPISODE 1**